1.0. **Majukumu ya Idara ya Elimu ya Juu**

Madhumuni ya jumla ya Idara ya Elimu ya Juu ni kuhakikisha maendeleo ya Sera ya Elimu ya Juu na uhamasishaji wa rasilimali na kuimarisha ufikiaji na Usawa. Majukumu ya idara ni kama ifuatavyo:

1.1. Kutayarisha, kuandaa, kufuatilia, kutathmini na kupitia upya utekelezaji wa Sera za Elimu ya Juu;

1.2. Kuanzisha, kufuatilia, na kutathmini utekelezaji wa Mipango na Miradi ya Wizara ya Elimu ya Juu;

1.3. Kuchochea maendeleo ya Elimu ya Juu ili kukidhi mahitaji ya Dunia ikiwa ni pamoja na kushauri kuhusu uwiano wa Elimu ya Juu kwa mahitaji ya kimaendeleo ya jamii;

1.4. Kuwasiliana na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) na Baraza la Taifa la Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) na Vyombo vingine vya taaluma kwa maendeleo ya ubora na stadi za Elimu ya Juu nchini;

1.5. Kuwasiliana na Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki na Vyuo Vikuu vingine vya Kikanda katika kukuza na kudumisha ushirikiano wa Kikanda na Ushirikiano wa Kimataifa katika Elimu ya Juu; na

1.6. Kukuza uelewa wa umma juu ya kazi na jukumu la sekta ya elimu ya Juu.

Idara itaongozwa na Mkurugenzi na Wakurugenzi Wasaidizi wawili (2): yaani Mkurugenzi Msaidizi Ufuatiliaji na Mkurugenzi Msaidizi Maendeleo.

2.0. **Takwimu: Idadi ya Vyuo Vikuu,**

2.1. Tanzania vipo Vyuo Vikuu 60.

2.1.1. Vyuo 32 vina usajili kamili (Umma 12 na Binafsi 20)

2.1.2. Vyuo Vikuu Vishiriki vipo 17 (Umma 07 na Binafsi 10)

2.1.3. Kampasi za Vyuo Vikuu, Vituo na Taasisi zipo 11 (Umma 03 na Binafsi 08)

3.0. **Takwimu ya Usajili katika Vyuo Vikuu**

3.1. Idadi ya wanafunzi waliosajiliwa kwa mwaka 2022/2023 ni 240,523

3.2. Usajili katika Vyuo Vikuu (Umma 162,553 na Binafsi 77,970)

4.0. **Taarifa ya Miradi**

4.1. **Malengo ya Mradi**

Idara inasimamia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi wenye malengo yafuatayo:

4.1.1. Kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika Taasisi za Elimu Juu kwa kufanya upanuzi na ujenzi wa Miundombinu;

4.1.2. Kuhuisha Mitaala katika program za kiapaumbele;

4.1.3. Kuwezesha mafunzo ya wanataalamu katika taasisi za Elimu za Juu; na

4.1.4. Kuwezesha matumizi ya Tehema katika Taasisi za Elimu za Juu kwa kuboresha miundombinu ya Tehama.

4.2. **Walengwa**

Walengwa wa Mradi wa HEET ni Taasisi za Elimu ya Juu (Vyuo Vikuu wa Serikali, HESLB, TCU and COSTECH na Taasisi tano chini ya Wizara ya Fedha zinazotoa elimu ya juu.

4.3. **Mfadhili**

Fedha za utekelezaji wa Mradi wa HEET ni mkopo wa serikali kutoka Benki ya Dunia

4.4. **Mipango wa Utekelezaji**

Mradi wa HEET ni Mradi unaotekelezwa kwa miaka mitano (2021/2022-2025/2026). Kila taasisi nufaika inatekeleza mradi kulingana malengo ya maandikoya Mradi aliyokusudiwa kutekelezwa katika taasisi husika.

4.5. **Matokeo tarajiwa**

4.5.1. Mitaala zaidi ya 300 katika program ya Kipaumbele kuandaliwa;

4.5.2. Wanataaluma wapatao 550 watapata mafunzo katika ngazi za shahada ya umahili na Uzamivu;

4.5.3. Zaidi ya watumishi 350 watakuwa wamepata mafunzo wezeshi yam da mfupi;

4.5.4. Taasisi za Elimu ya Juu kuwa na Miundombinu wezeshi ya kujifunza na kufundishia, Matumizi ya TEHAMA kama nyenzo ya kuongeza ufanisi

katika kufundisha na kujifunza na uboreshaji wa utoaji wa huduma kwa wateja.

4.5.5. Kuimarika kwa ushiriki wa viwanda/waajiri katika utekelezaji mradi hususani uandaaji na uhuishaji wa mitaala iendane na soko la ajira na mahitaji ya taifa.

4.6. **Mikataba ya utendaji na miongozo mbalimbali** (ambayo ni wazi kwa Umma)

4.6.1. Maandiko ya kuidhinishwa kwa Mradi na Utekelezaji wake (PAD &PoM)

4.6.2. Mwogozo wa Mazingira na Masuala ya Jamii,

4.6.3. Mwongozo wa usimamizi wa masuala ya jinsia na elimu jumuishi

4.6.4. Mwongozo wa Utoaji Ufadhili kwa Programu Maalumu kwa Wanafunzi wa Kike Waliopungukiwa na Sifa za Moja kwa Moja za Kujiunga na Elimu ya Juu katika Fani za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STUH) ; na

4.6.5. Mwongozo wa usomeshaji wa Watumishi kutoka Vyuo Vikuu Binafsi

4.6.6. Mwongozo wa kusimamia wafanyakazi

4.6.7. Mkataba wa utekelezaji mradi baina ya WyEST na Taasisi nufaika na Mradi

## 5.0. Takwimu za Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu

5.1. Mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu hutolewa na kusimamiwa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB). Zifuatazo ni takwimu kwa mwaka wa fedha 2022/2023:

5.1.1. Utoaji wa mikopo katika mwaka wa fedha 2022/2023, fedha zote za mikopo jumla ya TZS 654 bilioni zimetolewa na Serikali.

5.1.2. Hadi 30 Juni, 2023, wanafunzi 202,016 walipangiwa mikopo ambapo wanafunzi 73,513 ni wa mwaka wa kwanza na wanafunzi 128,503 wanaoendelea.

5.1.3. Hadi kufikia 30 Juni, 2023 fedha zilizokusanywa zilikuwa TZS. 169.8 bilioni sawa na 87% ya lengo la kukusanya TZS 195 bilioni katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023.

## 5.2. Uratibu wa Ruzuku (Samia Skolashipu)

5.2.1. Kuanzia mwaka 2022/2023, Serikali, imetenga TZS 3.0 bilioni kwa ajili ya ‘skolashipu’ kwa wanafunzi wenye ufaulu wa juu zaidi kwenye mitihani ya Kidato cha Sita iliyoendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) katika tahasusi za sayansi ambao wamepata udahili katika programu za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM) kwenye vyuo vya Elimu ya Juu nchini.

5.2.2. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 jumla ya wanufaika 636 (99%) kati ya lengo la mwaka la wanafunzi 640 wa skolashipu hiyo wamepangiwa fedha kiasi cha TZS 2.9 bilioni.

5.2.3. Katika mwaka wa 2023/2024 Serikali imetenga kiasi cha Tshs. 6.7 Bilioni kwa ajili ya wanafunzi wanaoendelea na bachi ya pili ya ufadhili kwa wanafunzi 640 na kufanya jumla ya wanufaika katika kipindi cha miaka miwili kufika1276.

## 5.3. Mawasilano

Kwa mawasiliano zaidi tuandikie kupitia:

Barua pepe: dhe@moe.go.tz